



## Siri za Dunia ya Mbali



Ndani ya Mwezi wa Kwanza mwaka 2005, chombo cha uchunguzi cha Huygens kilikuwa kikitatiza katika anga lenye ukungu la mwezi wa Titan, ambao ni mwezi mkubwa wa sayari ya Safani. Chombo hiki kilikuwa ni cha pekee na cha kwanza kutua katika sayari ya mbali kutoka Duniani, kitu ambacho si cha kushangaza ukizingatia kilichukuwa miaka 7 kufika huko!

Titan ni moja kati ya sehemu zinazofanana na Dunia katika mfumo wa jua. Kama ilivyo kwa Dunia Titan ina tabaka la hewa, ingawa tabaka la hewa lake ni pana zaidi na limepanuka zaidi angani kuliko letu. Tabaka hili lenye ukungu linafunika uso wa Titan kwa rangi ya chungwa na kuuficha usionekane kwa macho yetu. Mpango wa Huygen's ulikuwa ni kufichua siri hii ambayo leo tunajua! Kupitia mamia ya picha zilizopiwa kutoka katika uso wa Titan

Hivi sasa ni karibu miaka 8 tangu tukio hilo lilipotokea, na bado wanasayansi wanazidi kuchunguza dunia hii ya ajabu kupitia chombo cha Huygen kama jicho lao. Ilichukua sekunde kumi za makashikashi tangu chombo hiki kilipoingia katika anga, kudunda kwenye ardhi, kuburuzika na hatimaye kusimama. Wanasayansi kukofa katika European Space Agency wametengeneza modeli ya computa kuonyesha ni kwa jinsi gani kutua huku kuliweza kutokea.

Mda huu mfupi uliweza kuonyesha siri mpya kuhusu uso wa Titan. Kwa jinsi chombo hiki kilivyokuwa kinatembea wakati kilipotua, kilichonyesha tabaka jembamba la barafu katika uso wa Titan. Chini ya tabaka hilo ardhi ilikuwa kama mchanga ulio loa unaopatikana katika fukwe za hapa Duniani.

## COOL FACT

Titan ni mwezi wa pili kwa ukubwa katika mfumo wa jua, ni mkubwa zaidi ya mwezi wetu na ni mkubwa zaidi ya sayari Zebaki.

